**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**FUNGU 46**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI DESEMBA, 2025 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**JANUARI, 2026**

**YALIYOMO**


*SURA YA KWANZA* ______ 1

*MAJUKUMU NA VIPAUMBELE VYA WIZARA* ______ 1

*1.0. Utangulizi* ______ 1

*1.1. Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia* ______ 1

*1.2. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2025/26* ______ 2

*SURA YA PILI* ______ 6

*MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI* ______ 6

*2.0. Utangulizi* ______ 6

*2.1. Makusanyo ya Maduhuli kuanzia Julai 2025 hadi Desemba 2025* 6

*2.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara* ______ 7

*2.2.1. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/26* ______ 7

*2.2.2. Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo* ______ 8

*SURA YA TATU* ______ 10

*UTEKELEZAJI WA MAKUJUMU YA WIZARA* ______ 10

*3.0. Utangulizi* ______ 10

*3.1. Kuendelea na Utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Kuandaa Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo Nchini* ______ 10

*3.2. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali.* ______ 14

*3.3. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu* ______ 19

*3.4. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu* ______ 26

*3.5. Kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda* ______ 33

*3.6. Changamoto na Namna ya Utatuzi* ______ 38

*3.7. Hitimisho* ______ 40

*VIAMBATISHO* ______ 41

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AI | Artificial Intelligence |
| AJDP | African Journal of Development Perspectives |
| ARU | Ardhi University |
| ATC | Arusha Technical College |
| BRELA | Business Registration and Licensing Agency |
| COSTECH | Commission for Science and Technology |
| EASTRIP | East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project |
| ESMIS | Education Sector Management Information System |
| ESPJ | Education and Skills for Productive Jobs |
| FDCs | Folk Development Colleges |
| GPE - LANES | Global Partnership for Education - Literacy and Numeracy Education Support |
| HEET | Higher Education for Economic Transformation |
| HPGe | Hyper Pure Germanium |
| IAEA | International Atomic Energy Agency |
| IIT | India Institute of Technology |
| IMTC | Inter-Ministerial Technical Committee |
| IPT | Industrial Practical Training |
| JACCE | Journal of Applied Computing and Communication Engineering |
| JCIAF | Journal of Current Issues in Accounting and Finance |
| JIRCAS | Japan International Research Center for Agricultural Sciences |
| MAKISATU | Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology |
| NIDA | National Identification Authority |
| NTA | National Technical Award |
| OWM - TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| SEZ | Special Economic Zone |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| SSE | Samia Extended Scholarship |
| STI | Science, Technology and Innovation |

| | |
|---|---|
| TANZSTIP | Tanzania National Science, Technology and Innovation Platform |
| TCU | Tanzania Commission of Universities |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| UDSM | University of Dar Es Salaam |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |

**Orodha ya Majedwali**

Jedwali 2. 1: Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli ................................................ 6
Jedwali 2. 2: Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida ya Idara, Vitengo na Taasisi . 7
Jedwali 2. 3: Taarifa ya Fedha za Maendeleo ........................................................ 9

Jedwali 3. 1: Changamoto na Namna ya Utatuzi .................................................. 38

Kiambatisho Na. 1: Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli kwa Idara na Taasisi ...... 41
Kiambatisho Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Mishahara (PE) Taasisi .................... 54
Kiambatisho Na. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC) kwa Taasisi ........................................................................................................ 58
Kiambatisho Na. 4: Mchanganuo wa Bajeti ya Shughuli za Maendeleo.................... 60

**Muundo wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Kipindi cha Nusu Mwaka Julai hadi Desemba 2025**

Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti inajumuisha Makadirio, Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi Julai hadi Desemba 2025 kwa mwaka wa Fedha 2025/26. Aidha, taarifa hii imejumuisha taarifa za utekelezaji kutoka katika Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Taarifa imegawanyika katika sura tatu (3) kama ifuatavyo:

(i) **Sura ya kwanza**: Utangulizi unaoelezea Majukumu na Vipaumbele vya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(ii) **Sura ya Pili:** Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ikiainisha Makadirio ya Mapato na Matumizi na utekelezaji wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kutoka Julai 2025 hadi Desemba 2025 katika mwaka wa fedha 2025/26; na

(iii) **Sura ya Tatu**: Utekelezaji wa jumla wa majukumu katika ngazi ya Idara, Vitengo, Taasisi na miradi kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025 kulingana na malengo na vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na changamoto na mbinu zilizotumika kukabiliana nazo.

## SURA YA KWANZA

## MAJUKUMU NA VIPAUMBELE VYA WIZARA

### 1.0. Utangulizi

Sehemu hii inaelezea majukumu ya Wizara kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mawaziri Sura 299 kupitia Tangazo la Serikali Na. 686 la tarehe 19 Desemba, 2025. Aidha, sehemu hii inabainisha vipaumbele vya Wizara katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26.

### 1.1. Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Majukumu ya Wizara kwa kuzingatia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Uwaziri Sura 299, Tangazo la Serikali Na. 686 la tarehe 19 Desemba, 2025 ni kama ifuatavyo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu nchini kwa kuandaa Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali kutoka ngazi ya Elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu. Vilevile, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika nyanja mbalimbali ikiwemo Biashara, Viwanda, Kilimo na maisha ya kila siku. Wizara pia inawajibika katika uendeshaji wa Elimu ya Ualimu, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia mafungu mawili (2) ambayo ni Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia) na Fungu 18 (Tume ya Taifa UNESCO).

Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yameainishwa katika Hati Idhini, GN No. 686 ya tarehe 19 Desemba, 2025 ambapo Wizara imeelekezwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo na Ujuzi;

(ii) kusimamia maendeleo ya Elimumsingi;

(iii) kusimamia ithibati ya Elimu ya Ualimu na maendeleo ya viwango vya Elimu ya Ualimu;

(iv) kusimamia maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(v) kusimamia maendeleo ya Elimu ya Juu;

(vi) kubaini na kuendeleza vipaji;

(vii) kusimamia utoaji wa elimu ya maendeleo kwa wananchi;

(viii) kusimamia Mfumo wa Tuzo wa Taifa;

(ix) kusimamia ubainishaji na uendelezaji wa ujuzi unaohitajika;

(x) kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule;

(xi) kusimamia huduma ya uchapaji wa nyaraka za elimu;

(xii) kuhamasisha matumizi ya Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;

(xiii) kuendeleza utaalamu asilia katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(xiv) kusimamia masuala ya Tume ya Taifa ya UNESCO;

(xv) kuratibu na kusimamia utafiti na maendeleo katika Sayansi na Teknolojia;

(xvi) kuimarisha utendaji na maendeleo ya rasilimaliwatu katika Wizara; na

(xvii) kusimamia Idara, Mashirika, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

## 1.2. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2025/26

Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imejielekeza kutekeleza yafuatayo:

**a. Kuendelea na utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Kuandaa Miongozo na Kutoa Mafunzo Nchini**

(i) Kuendelea na uandaaji wa zana za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhuisha na kuandaa miongozo mbalimbali ya utoaji elimu na mafunzo nchini, kukamilisha Mfumo wa Taifa wa Upimaji na Tathmini (National Assesment Framework) na kuandaa Mfumo wa Taifa wa Mitaala (National Curriculum Framework);

(ii) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 na sheria tisa (9) katika taasisi ambazo ni COSTECH, TLSB, NECTA, TEWW, VETA, TCU, NACTVET, TIE na TEA ili ziendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023 na Sheria za Kikanda na Kimataifa;

(iii) Kuendelea na maboresho ya mitaala ngazi ya elimu ya Amali (Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi) na Elimu ya juu kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu wa ngazi hizo;

(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa umma na watendaji kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu, Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu;

(v) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia (1996) ili kuwa na sera inayoakisi hali halisi na mahitaji ya sasa katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

(vi) Kukamilisha mapitio ya Muundo na Majukumu ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha ufanisi na mchango wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali**

(i) Kuimarisha Chuo cha Ualimu Mtwara (K) na Mtwara (U) kuwa Vyuo vya mafunzo ya Ualimu wa Ufundi;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa VETA 64 za Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe;

(iii) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya VETA 98 na FDC 54;

(iv) Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Stashahada kutoka 8,000 wanaoendelea hadi kufikia 10,000 wa mwaka wa kwanza katika fani za sayansi na ufundi;

(v) Kuanza ujenzi wa vyuo vitano (5) vya ufundi (Polytechnics college); na

(vi) Kuendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Kituo cha Magonjwa ya Moyo - Mloganzila.

**c. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu**

(i) Kuwezesha ujenzi wa madarasa 1,549 (awali 600, msingi 500 na sekondari 449); mabweni 55 kwa shule za sekondari kwa ajili ya utoaji wa elimu jumla;

(ii) Kuendelea kuimarisha mafunzo kazini na tarajali kwa walimu, wakufunzi na wasimamizi wa elimu nchini;

(iii) Kuendelea kuimarisha Uthibiti wa Ubora wa Shule kwa kuwapatia vitendea kazi;

(iv) Kuendelea kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari pamoja na kuimarisha huduma ya maktaba za jamii kwa ununuzi wa vitabu; na

(v) Kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu maalum na jumuishi kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji, mafunzo, uandaaji wa miongozo kwa ngazi zote za elimu na kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 2,000 watakaosoma Diploma ya Ualimu wa Elimu Maalum.

**d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

(i) Kuongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka 245,314 mwaka 2024/25 hadi wanafunzi 252,773 (mwaka wa kwanza 88,320 na wanaoendelea 164,453) kwa mwaka 2025/26;

(ii) Kuendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo ya Sayansi kupitia *SAMIA Skolashipu* 2,630 (ikiwemo wanafunzi 1,220 wa mwaka wa kwanza, wanafunzi 80 wa Shahada za Umahiri, 1,330 wanaoendelea);

(iii) Kuendelea kutoa ufadhili kupitia ***SAMIA Extended Skolashipu*** kwa ajili ya Shahada za Juu ikiwemo eneo la sayansi na teknolojia ya nyuklia;

(iv) Kutoa ufadhili kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika matokeo ya Kidato cha Sita kwenye michepuo ya sayansi ili kujiunga na Shahada ya Kwanza katika eneo la TEHAMA kupitia Extended Skolashipu. Katika hili juhudi zaidi zitatumika kupeleka vijana wa kitanzania kusomea mambo ya kompyuta na akili-unde kwenye vyuo bora vilivyo nje ya nchi;

(v) Kuendelea kugharamia mafunzo kwa wanataaluma katika ngazi ya umahiri na shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali katika vyuo vikuu nchini;

(vi) Kumalizia ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu; na

(vii) Kuendelea kutoa tuzo kwa watafiti watakaochapisha matokeo ya utafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

(i) Kuimarisha uratibu, usimamizi, na uwekezaji katika Sayansi, Teknolojia, na Ubunifu kati ya Wizara za kisekta na Halmashauri ili kuongeza ufanisi, ushirikiano na kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(ii) Kuwekeza kwenye miundombinu ya kitaifa ya utafiti na ubunifu ili kuchochea uvumbuzi na ubiasharishaji wa teknolojia na bidhaa zenye mchango mkubwa kwa uchumi wa viwanda;

(iii) Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia za kidijiti katika ujifunzaji na ufundishaji kwa ngazi zote za elimu nchini;

(iv) Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Mahitaji ya Teknolojia katika sekta mbalimbali (National Technology Roadmap-2050);

(v) Kuimarisha taasisi za elimu ya juu na taasisi za kitafiti kuendelea kufanya utafiti wa kimkakati na kuongeza mchango wake katika agenda ya maendeleo ya Taifa;

(vi) Kuongeza idadi ya bunifu na teknolojia zilizoendelezwa na kuingia sokoni kutoka 42 hadi 55;

(vii) Kuendelea kuwawezesha wabunifu kuendeleza bunifu zao ili zifikie hatua ya ubiasharishaji; na

(viii) Kuimarisha uthibiti na utafiti wa kimkakati unaolenga kuongeza wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

## 2.0. Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ikiainisha taarifa ya makusanyo ya maduhuli, makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara katika matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2025. Aidha, muhtasari wa taarifa ya miradi ya maendeleo umetolewa katika *Kiambatisho Na. 4* cha taarifa hii.

## 2.1. Makusanyo ya Maduhuli kuanzia Julai 2025 hadi Desemba 2025

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zinakadiria kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 720,507,879,789.63.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,402,257,000.00** ni makusanyo ya Idara na Vitengo vya Wizara na **Shilingi 712,105,622,789.63** zitakusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni: ada, malipo ya ushauri elekezi, mchango wa uthibiti ubora wa shule na baadhi ya huduma zinazotolewa na wizara.

Hadi kufikia Desemba 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 309,157,900,922.67** sawa na asilimia **43** ya makadirio ambapo, **Shilingi 3,562,724,787.00** zimekusanywa na Idara na Vitengo, na **Shilingi 305,595,176,135.67** zimekusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Mchanganuo wa makusanyo umeainishwa katika *Jedwali Na. 2.1. na Kiambatisho Namba 1.*

*Jedwali 2. 1: Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli*

| Maelezo | Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka 2025/26 | Makusanyo Julai 2025 -Desemba 2025 | % ya Makusanyo |
|---|---|---|---|
| Idara na Vitengo | 8,402,257,000.00 | 3,562,724,787.00 | 42% |
| Taasisi zilizo chini ya Wizara | 712,105,622,789.63 | 305,595,176,135.67 | 43% |
| **Jumla** | **720,507,879,789.63** | **309,157,900,922.67** | **43%** |

### 2.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara

Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara pamoja na Taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,826,078,405,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 688,614,234,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara **Shilingi 635,249,992,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 53,364,242,000.00**) na **Shilingi 2,137,464,171,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fedha za ndani ni **Shilingi 1,186,987,965,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 950,476,206,000.00**). Mchanganuo wa Makadirio na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

#### 2.2.1. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kupitia Fungu 46 inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 688,614,234,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 635,249,992,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zake, ambapo **Shilingi 109,268,953,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Idara na Vitengo na **Shilingi 525,981,039,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Taasisi. Aidha, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 53,364,242,000.00** ambapo Matumizi Mengineyo kwa Idara na Vitengo ni **Shilingi 37,510,134,348.00** na Taasisi ni **Shilingi 15,854,107,652.00**.

Hadi kufikia Desemba, 2025 Wizara kupitia Fungu 46 imepokea jumla ya **Shilingi 328,949,792,928.61** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **48** ya bajeti ya **Shilingi 688,614,234,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 304,266,273,411.84** ni fedha za Mishahara (PE) na **Shilingi 24,683,519,516.77** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Mchanganuo wa makadirio na kiasi kilichopokelewa umeoneshwa katika *Jedwali Na. 2.2*

*Jedwali 2. 2: Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida ya Idara, Vitengo na Taasisi*

| **Maelezo** | **Makadirio 2025/26** | **Kiasi (Sh) Kilichopokelewa hadi Desemba, 2025** | **% ya kilichopokelewa** |
|---|---|---|---|
| **A: Matumizi ya Kawaida kwa Idara na Vitengo** | | | |
| Mishahara (PE) Idara na Vitengo | 109,268,953,000.00 | 52,629,334,862.00 | 48% |

| Maelezo | Makadirio 2025/26 | Kiasi (Sh) Kilichopokelewa hadi Desemba, 2025 | % ya kilichopokelewa |
|---|---|---|---|
| Matumizi Mengineyo (OC) | 37,510,134,348.00 | 16,876,851,829.64 | 45% |
| **Jumla** | **146,779,087,348.00** | **69,506,186,691.64** | **47%** |
| **B: Matumizi ya Kawaida kwa Taasisi** | | | |
| Mishahara (PE) yaTaasisi | 525,981,039,000.00 | 251,636,938,549.84 | 48% |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 15,854,107,652.00 | 7,806,667,687.13 | 49% |
| **Jumla** | **541,835,146,652.00** | **259,443,606,236.97** | **48%** |
| **C: Matumizi ya Kawaida kwa Idara, Vitengo na Taasisi** | | | |
| Mishahara (PE) | 635,249,992,000.00 | 304,266,273,411.84 | 48% |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 53,364,242,000.00 | 24,683,519,516.77 | 46% |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida kwa Idara, Vitengo na Taasisi** | **688,614,234,000.00** | **328,949,792,928.61** | **48%** |

### 2.2.2. Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo

Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/26 ni **Shilingi 2,137,464,171,000.00** ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 1,186,987,965,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 950,476,206,000.00**.

Hadi kufikia Desemba, 2025 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 648,727,894,880.44** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **30** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 454,978,352,359.34** ni fedha za ndani na **Shilingi 193,749,542,521.10** ni fedha za nje. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa umeainishwa katika *Jedwali Namba 2.3*

*Jedwali 2. 3: Taarifa ya Fedha za Maendeleo*

| **Maelezo** | **Makadirio 2025/26** | **Kiasi (Sh) Kilichopokelewa hadi Disemba, 2025** | **% ya kiasi kilichopokelewa** |
|---|---|---|---|
| Fedha za Ndani | 1,186,987,965,000.00 | 454,978,352,359.34 | 38% |
| Fedha za Nje | 950,476,206,000.00 | 193,749,542,521.10 | 20% |
| **Jumla ya Makadirio ya Maendeleo** | **2,137,464,171,000.00** | **648,727,894,880.44** | **30%** |

# SURA YA TATU

# UTEKELEZAJI WA MAKUJUMU YA WIZARA

## 3.0. Utangulizi

Sehemu hii inatoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya idara, vitengo, taasisi na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Desemba, 2025 kwa kuzingatia vipaumbele vitano (5) vilivyobainishwa katika bajeti ya mwaka 2025/26. Aidha, sehemu hii inabainisha changamoto za Wizara, namna ya utatuzi wake na hitimisho. Ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele vitano (5) vya Wizara:

## 3.1. Kuendelea na Utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Kuandaa Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo Nchini

Serikali imeendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 na marekebisho mbalimbali ya sheria za taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuendana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kwa kutekeleza yafuatayo :

(i) imekamilisha zoezi la kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu na kuandaa taarifa ya awali ya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 ikiwa ni hatua muhimu katika kufanya mapitio ya sheria husika ili kuendana na mahitaji ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023. Aidha, Wizara inaendelea na vikao maalumu vya wadau kwa ajili ya kuhakiki na kuthibitisha taarifa ya husika; na

(ii) imeandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba, marekebisho ya Sheria ya Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania, Kanuni za Sheria ya Baraza la Mitihani Tanzania na Mapitio ya Amri ya kuanzishwa kwa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) ili ziendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023;

Vilevile, Serikali imeendelea kuandaa mikakati mbalimbali na kuimarisha mifumo ya takwimu za elimu ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa rasimu ya Mkakati wa Ubia Baina ya Serikali na Sekta Binafsi Katika Elimu na Mafunzo (Public-Private Partnership Strategy for Education and Training in Tanzania - 2025/26 to 2029/30) kwa lengo la kuweka utaratibu madhubuti na mazingira wezeshi ya ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuboresha huduma, miundombinu na ubunifu katika Elimu;

(ii) imeandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan) ambao ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, kwa lengo la kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa sera kwa miaka mitano;

(iii) imekamilisha taarifa ya Mapendekezo ya Maandalizi ya Mapokezi ya makundi-rika mawili ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Elimu ya Sekondari ya Chini Mwaka 2028. Aidha, taarifa husika inabainisha mahitaji na kuweka mikakati inayohitajika katika kuwezesha mapokezi ya makundi-rika mawili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ifikapo mwaka 2028;

(iv) imefanya maboresho ya Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023, mitaala iliyoboreshwa ya Mwaka 2023, Dira ya Taifa ya 2050, Mpango wa Maendeleo katika Sekta ya Elimu (Education Eector Development Plan - ESDP) na Mpango Mkakati wa Wizara - 2026 /27 hadi 2030/31; na

(v) imekamilisha ujenzi na kuanza majaribio ya Mfumo wa Takwimu wa Sekta ya Elimu (Education Sector Management Information System – ESMIS) utakaowezesha upatikanaji wa takwimu zote za Sekta eneo moja kwa kujumuisha takwimu kutoka mifumo mingine ya Taasisi za Serikali ikiwemo NIDA, RITA, Wizara ya Mambo ya Nje, Uhamiaji, na OWM–TAMISEMI.

Serikali imeendelea na mapitio ya sera na miongozo inayosimamia utekelezaji wa masuala ya Sayansi, Utafiti, Teknolojia na Ubunifu nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini ya maudhui ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010), Sera ya Taifa ya Teknolojia (2013) na kuandaa taarifa ya mapendekezo inayobainisha umuhimu wa kuwa na Sera moja inayoakisi hali halisi na mahitaji ya sasa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

(ii) imekamilisha rasimu za miongozo/viunzi mbalimbali vinavyolenga kuimarisha maendeleo na mchango wa Utafiti na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU), ikiwemo: Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Ubunifu na Teknolojia vya Mkoa (Regional Innovation and Technology Support Centres); Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Maabara za Rufaa za Taifa za Utafiti na Ubunifu wa Viwanda (National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories); Kiunzi cha Kitaifa cha uboreshaji wa Teacher Resource Centers ili zitumike kama Kumbi za STEM na Teknolojia za Kidijitali (DigiSTEM Hubs); pamoja na Kiunzi cha Kitaifa cha Uanzishaji na Uendeshaji wa Ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Teknolojia za Kidijitali katika Sekta ya Elimu (National edTech Partnership and Adoption Framework–NEPAF).

Serikali imendelea kuhuisha na kuandaa viunzi na miongozo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Kiunzi cha Taifa cha Tathmini ya Elimu (Tanzania National Education Assessment Framework) kwa lengo la kuimarisha tathmini ya elimu na mafunzo nchini;

(ii) meandaa rasimu ya Kiunzi cha Taifa cha Mitaala (National Curriculum Framework);

(iii) imekamilisha rasimu ya Kiunzi cha Mafunzo ya Ualimu Kazini kabla ya Ajira (Teachers Internship Framework);

(iv) imechapa na kusambaza Kiunzi cha Umahiri wa Walimu katika TEHAMA (ICT Competency Framework for Teachers) kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia;

(v) imeandaa Kiunzi cha Mnyororo wa Uandaaji na Usambazaji Vitabu shuleni kwa lengo la kuhakikisha vitabu vyenye viwango stahiki vinapatikana shuleni kwa wakati;

(vi) imehuisha mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la mwaka 2023;

(vii) imehuisha Mwongozo wa Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (Teaching Practice Guideline) kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika mafunzo ya ualimu;

(viii) imeandaa Mwongozo wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule na Vituo vya Walimu, 2025 kwa ajili ya kuweka utaratibu na mfumo wa utoaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) katika ngazi ya shule na vituo vya walimu ili kuimarisha ubora wa walimu na elimu nchini;

(ix) imeandaa rasimu ya Mwongozo wa uratibu na usimamizi wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa lengo la kuimarisha uendeshaji wa programu za elimu ya watu wazima na elimu ya nje ya mfumo rasmi;

(x) imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Elimu kwa njia ya Masafa kwa Walimu ngazi ya Stashahada ili kutoa fursa ya mafunzo ya ualimu kwa njia ya masafa;

(xi) imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Shule zinazotumia Mtaala wa Kimataifa kwa lengo la kuweka utaratibu maalumu wa uendeshaji wa shule husika;

(xii) imeandaa Mwongozo wa Kitaifa kuhusu Fursa za Ufadhili wa Masomo wa Ndani na Nje ya Nchi. Lengo ni kuwezesha Watanzania kupata elimu bora inayolingana na viwango vya kimataifa;

(xiii) imeendelea kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Utambuzi na Uendelezaji wa Vipawa, Vipaji na Ubunifu katika ngazi zote za Elimu kwa lengo la kubaini na kuwaendeleza wanafunzi wenye uwezo wa kipekee katika taaluma au ubunifu;

(xiv) imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Usajili na Utoaji wa Leseni kwa Walimu wote walioajiriwa na serikali na shule zisizo za serikali kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi;

(xv) imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Ufundishaji kwa Walimu Wanafunzi Wakati wa Mafunzo kwa Vitendo (Teaching under Supervision Guideline for Intern Teachers) kwa lengo la kutoa maelekezo ya uendeshaji na usimamizi wa mafunzo kwa vitendo (Internship) kwa walimu na wadau wengine; na

(xvi) imeandaa rasimu za miongozo 4 ambayo ni Mwongozo wa Sanaa na michezo rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum Mwongozo wa matumizi ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Mwongozo wa Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na Mwongozo wa utoaji wa elimu ya amali kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi.

## 3.2. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali.

Serikali imeendelea kuongeza fursa kwa kuboresha miundombinu ya shule za sekondari za amali, vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya vyuo 56 vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo vyuo vya elimu ya ufundi ni 27 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 29. Aidha, imeidhinisha kuanzishwa kwa idara/programu 27 katika vyuo 20 ili kuendesha programu za NTA;

(ii) imeratibu udahili wa wanafunzi 179,036 (wanawake 86,448 na wanaume 92,588) wanafunzi wa vyuo vya serikali ni 100,883 (wanawake 48,959 na wanaume 51,924);

(iii) imedahili vijana 918 wanaotoka katika mazingira magumu katika vyuo vya VETA hususan wasichana waliopata ujauzito katika umri mdogo. Aidha, imedahili wanafunzi 47 (wanaume 29 na wanawake 18) wenye ulemavu;

(iv) imerasimisha ujuzi kwa wanagenzi 656 (wanawake 384 na wanaume 272) kupitia programu ya WEZESHA BINTI katika mkoa wa Kigoma;

(v) imeanza ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Ualimu Mtwara (K) na Mtwara (U) Ndaki ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya –MUST ambapo hadi Desemba 2025 wanafunzi watano (5) wamedahiliwa katika Shahada ya Elimu Ufundi katika Uhandisi wa ujenzi;

(vi) imeendelea na ujenzi wa VETA 64 za wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe ambapo wastani wa ujenzi umefikia asilimia 67 kwa vyuo 64 vya wilaya na asilimia 68 kwa chuo cha Mkoa wa Songwe;

(vii) imeanza maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vitano (5) vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (Polytechnics) katika mkoa wa Mtwara, Kigoma, Mwanza, Morogoro na Unguja-Zanzibar ili kupokea wanafunzi wa sekondari za amali; na

(viii) imeendelea na ujenzi wa karakana ya uzalishaji *(Industrial workshop) ,* ujenzi wa msingi (*substructure*) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 43 kupitia awamu ya pili ya mradi wa ***KUHN International Projects (KIP)***. Aidha, imeendelea na ujenzi wa hospitali na ununuzi wa vifaa tiba kwa lengo la kutoa mafunzo ya vitendo kupitia kozi ya biomedical pamoja na kutoa huduma za afya kwa wafanyakazi na wananchi wa maeneo jirani, ambapo ujenzi wa hospitali umefikia asilimia 96 na ununuzi wa vifaa tiba ulitengwa katika awamu tatu ,vifaa tiba awamu ya kwanza imefikia asilimia 100 katika chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

Serikali imeendelea kuboresha vituo vya umahiri ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, na Chuo cha Ufundi Arusha kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Ufundi Arusha - ATC Kampasi ya Kikuletwa. Aidha, inaendelea na ufungaji wa mitambo kwa ajili

ya kuzalishia umeme kufundishia na kujifunzia katika Kampasi ya Kikuletwa. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme (Hydropower Plant) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 60;

(ii) imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika katika Taasisi ya Teknolojia - DIT Kampasi ya Dar es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 99 na ujenzi katika Kampasi ya Mwanza umefikia asilimia 88;

(iii) imekarabati miundombinu ya ufundishaji katika Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere Kampasi ya Pemba. Aidha, imeendelea na ujenzi wa hosteli mbili (moja wanaume na moja wanawake) katika Kampasi ya Karume Zanzibar zenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 768 kila moja. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 52. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa maktaba itakayotumika na wanafunzi 2,500 pamoja na ukumbi wa mihadhara utakaoweza kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika Kampasi ya Kivukoni ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 47;

(iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi wa mihadhara (Lot 2) katika Kampasi ya Pemba ambapo ujenzi umefikia asilimia 60;

(v) imeendelea na ujenzi wa bwalo la chakula katika Kampasi ya Karume ambapo ujenzi umefikia asilimia 91, Kampasi ya Pemba ujenzi wa bwalo umefikia asilimia 75. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa madarasa na ofisi katika kampasi ya kivukoni ambapo ujenzi umefikia asilimia 50;

(vi) imenunua vifaa na mitambo ya kisasa ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Teknolojia - DIT Kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza ambapo utekeleza wake umefikia asilimia 18; na

(vii) imewajengea uwezo wakufunzi 32 kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na Chuo cha Ufundi Arusha kuhusu mafunzo ya viwandani (Industrial Attachment) ili kuboresha ubora wa mafunzo yanayotolewa katika sekta za kipaumbele.

Serikali imeendelea kuwezesha mafunzo kwa vitendo viwandani (Industrial Practical Training – IPT) na huduma ya chakula kama ifuatavyo:

(i) Imewezesha jumla ya wanafunzi 9,670 kushiriki mafunzo kwa vitendo viwandani, ambapo kati yao wanafunzi 538 ni wa ngazi ya stashahada wanaofadhiliwa na Serikali. Aidha, maandalizi ya wanafunzi 959 kushiriki mafunzo kwa vitendo viwandani mwezi Januari 2026 yanaendelea katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya- MUST;

(ii) imewezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,619 kutoka taaluma ya ualimu na wanafunzi 5,150 kutoka taaluma zisizo za ualimu katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; na

(iii) imeendelea kutekeleza mikataba ya ushirikiano 49 kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa vyuo vya ufundi na viwanda na Taasisi za ndani na nje ya nchi.

Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na uthibiti katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa ithibati kwa vyuo 19 vya Elimu ya Ufundi - TET na programu 31 za vyuo vya elimu ya ufundi stadi - VET ili kuwezesha wahitimu katika vyuo hivyo kupata mafunzo yenye ubora unaostahili na shindani katika soko la ajira na kujiajiri;

(ii) imehakiki mitaala 114 (Elimu ya ufundi 87 na Elimu ya mafunzo ya ufundi stadi 27) iliyokuzwa na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi soko la sasa na la baadaye;

(iii) imeidhinisha na kuanzisha idara/programu 27 katika vyuo 20 ili kuendesha programu za National Technical Award-NTA;

(iv) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika vyuo vya elimu ya ufundi 106 na shule za sekondari za amali 38. Katika ufuatiliaji huo ushauri juu ya namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ulitolewa. Aidha, vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilichukuliwa hatua stahiki kama kufutiwa usajili na kusimamishwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika;

(v) imekamilisha ukarabati wa jengo la mgahawa wa watumishi katika ofisi ya Kanda ya Mashariki – Dar es Salaam; na

(vi) imekamilisha kuhuisha mfumo wa TVETIMS na sasa upo katika hatua ya majaribio.

Serikali imeendelea kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha utekelezaji wa Programu ya Mafunzo Jumuishi ya Kukuza Ujasiriamali (Integrated Training for Enterpreneurship Promotion – INTEP) ambapo wanufaika 729 (wanaume 324 na wanawake 405) walipatiwa mafunzo;

(ii) imewajengea uwezo walimu 36 kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa Uanagenzi Pacha katika vyuo vya Kagera RVTSC, Shinyanga VTC na Dodoma RVTSCc;

(iii) imewezesha watumishi 18 wa Baraza la Taifa la Elimu ya Fundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwenda mafunzo ya muda mrefu (Shahada ya Uzamivu 7; Shahada ya Uzamili 7; Shahada ya Kwanza 4) katika vyuo mbalimbali nchini; na

(iv) imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wakufunzi 10 (Chuo cha Ufundi Arusha 4 na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam 6) na mafunzo ya muda mfupi kwa wakufunzi 13.

## 3.3. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu

Serikali imeendelea kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa Elimu ya awali msingi, sekondari na ualimu kwa kutekeleza yafuatayo;

(i) imesajili shule 291 kwa mchanganuo ufuatao; awali pekee 16 zisizo za serikali, awali na msingi 122 (Serikali 38 na zisizo za Serikali 84), Sekondari 151 (Serikali 117 na zisizo za Serikali 34), na vyuo 2 vya Ualimu (kisicho cha Serikali 1 na Serikali 1);

(ii) imedahili wanafunzi wa ualimu 11,065 (wanawake 3,983 na wanaume 7,082) kati yao wanafunzi wa vyuo vya ualimu vya Serikali ni 7,157(wanawake 2,576 wanaumme 4,581) na visivyo vya Serikali ni 3,908 (wanawake 1,407 na wanaume 2,501);

(iii) imewezesha ujenzi wa mabweni sita (6) katika shule za sekondari, madarasa 128 (sekondari 62 na msingi 66); matundu ya vyoo 5,115 (sekondari 123 na msingi 4,992); bwalo la chakula; nyumba ya mwalimu; na ukarabati wa shule mbili (2) za sekondari;

(iv) imefanya tathmini ya asasi 3,947 kati ya 6,962 ambapo shule za awali na msingi 2,861; shule za sekondari ni 1,036; na vyuo vya elimu na mafunzo 19, vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi 22 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 9 ambapo asasi zilizobainika kuwa na mapungufu zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(v) imefanya tathmini maalumu katika asasi 911 (za Serikali 640 na zisizo za Serikali 271). Aidha, Asasi 377 zilifanyiwa Tathmini ya Usajili ambapo 187 ni za serikali na zisizo za serikali ni 190;

(vi) imefanya tathmini ya wa matumizi ya TEHAMA na teknolojia saidizi katika shule 15 za msingi zinazopokea wanafunzi wenye uziwikutokuona kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa Kundi hili. changamoto zilizobainishwa zimetatuliwa kwa kununua vifaa vya TEHAMA na teknolojia

saidizi ili kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kujifunza kwa ufanisi;

(vii) imefanya tathmini ya uchapaji na ugawaji wa vitabu vya braille na maandishi yaliyokuzwa kwa wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu shule jumuishi za msingi 15 na sekondari 10 na kubaini uwepo, uhifadhi na matumizi sahihi ya vitabu katika ngazi hizo za elimu;

(viii) imefanya tathmini ya shule kongwe 27 za msingi na sekondari 26 zinazotoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili tathmini hiyo imesaidi kubaini changamoto mbalimbali katika shule hizo ikiwemo uhaba wa vifaa, na miundombinu wezeshi katika utekelezaji wa elimu jumuishi. tathmini hii imesabaisha ununzi wa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitjia malum kama viti mwendo, l*aptops*, fimbo nyeupe na *embosser machine*. ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji;

(ix) imefanya tathmini ya tuhuma katika asasi 115 zikiwemo za Serikali 72 na zisizo za Serikali 43, na ziara ya kuona uendeshaji wa asasi ilifanyika katika asasi 419 zikiwemo za Serikali 381 na zisizo za Serikali 38 ambapo ushauri wa kitaalamu na kitaaluma ulitolewa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa elimu bora;

(x) imefanya tathmini ya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika asasi 677 kati ya 1,260 zikiwemo shule za Awali na Msingi 523; shule za Sekondari ni 153, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi 1 ambapo asilimia 35 zimefanya mabadiliko chanya ya viwango vya ubora baada ya kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla;

(xi) imefanya tathmini ya ufundishaji wa somo la elimu jumuishi na Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) katika vyuo vya ualimu vya Serikali 35 na binafsi 13 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa darasa jumuishi katika shule za msingi. Tathmni hii imebaini masomo haya yanafundishwa katika vyuo vyote vya serikali na visivyo vya serikali. Aidha ushauri wa kitaalam ulitolewa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(xii) imewezesha mafunzo kwa walimu 3,602 wa shule za msingi kuhusu mpango wa Shule Salama kwa lengo la kuboresha huduma za malezi, ushauri na unasihi shuleni;

(xiii) imetoa mafunzo kwa viongozi wa elimu 5,297 (wanaume 3,663 na wanawake 1,634) kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Motisha kwa Walimu kwa mchanganuo ufuatao; Maafisa Elimu Kata 3876, Wakurugenzi wa Halmashauri 137, Maafisa Elimu 363, Maafisa Taaluma 363, Wathibiti Ubora wa Shule wa Wilaya 184, Makatibu wa Tume ya Walimu 153, Maafisa Utumishi 172, Maafisa Elimu Mkoa na Maafisa Taaluma 49;

(xiv) imetoa mafunzo kwa watekelezaji wa elimu jumuishi 327 ambao ni ubainishaji za mikoa wakiwemo: wabainishaji kwa ajili ya shule za msingi 224. Aidha, katika ngazi ya taasisi za elimu ya juu imetoa mafunzo kwa maafisa maktaba, wakutubi, maabara, 55. Vilevile, washauri wa wanafunzi, maafisa mitihani, maafisa ratiba wasajiri na waratibu wa elimu jumuishi wahuduma 48 wamepata mafunzo. Mafunzo haya yalilenga kuimarisha ubainishaji na utoaji wa huduma jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(xv) imetoa mafunzo ya uongozi bora kwa maafisa elimu mikoa 26, maafisa elimu wilaya 182 na waratibu elimu Kata 1,960 kwa lengo la kuimarisha umahiri wa maafisa elimu katika kusimamia utekelezaji wa Sera;

(xvi) imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa walimu 1,972 katika kozi za Astashahada, Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu, na Uthibiti Ubora wa Shule katika Kampasi za Bagamoyo, Mbeya na Mwanza kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu – ADEM;

(xvii) imesahihisha insha 475 za wanafunzi katika mashindano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki-EAC kwa wanafunzi wa shule za sekondari ambapo insha za wanafunzi 263 (wasichana 140 na wavulana 123) zilikuwa na sifa. Lengo la mashindano hayo ni kuwajengea uwezo wanafunzi katika kujieleza;

(xviii) imefanya uhamasishaji kuhusu uandikishaji wa watoto wenye ulemavu unaoanza Oktoba 2025 hadi Machi 2026 kupitia maadhimisho ya siku ya watu

wenye ulemavu, siku ya viziwi, wenye ualbino, fimbo nyeupe na *braille* kitaifa ambapo watu 8,201 walishiriki. Aidha, kuelezea juu ya mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023 pamoja na kuelezea mafanikio ya serikali katika kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum hususan shule ya nyumbani (home schooling); na

(xix) imefanya Maadhimisho ya Siku ya Kisomo Kimataifa na Juma la Elimu ya Watu Wazima tarehe 15 -19/09/2025 Mkoani Katavi ambapo takribani washiriki 1,000 walihudhuria.

**Upatikanaji wa Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Serikali, imeendelea kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuimarisha uwiano wa Kitabu kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha uandaaji wa vitabu vya masomo ya Hisabati na Sayansi kwa Kidato cha kwanza katika mfumo wa kidijitali na inaendelea na uandaaji wa vitabu vya masomo ya kidato cha pili. Aidha, imesambaza vitabu vya sekondari katika halmashauri zote za Tanzania bara;

(ii) imeendelea na uchapaji wa nakala 4,048,071 za vitabu vya kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo ya sekondari kidato cha 2 na 3 kwa mkondo wa amali na mkondo wa jumla, vitabu vya maandishi ya Braille kwa shule za msingi na sekondari na vitabu vya kiada kwa shule za msingi darasa la V;

(iii) imekamilisha uandishi wa aina 45 za vitabu vya sekondari mkondo wa Amali kwa ajili ya kidato cha 3, kidato cha 1, kidato cha 2 na muhtasari;

(iv) imeandaa aina 26 ya vitabu vya kidato cha 6, kiongozi cha mwalimu 26 na vitabu vya Amali 47 vya kidato cha 3 ambapo vitabu hivyo vipo katika hatua ya uchapaji. Vilevile, imehakiki miswada 34 ya vitabu vya ziada kutoka kwa wachapishaji binafsi;

(v) imechapa nakala za vitabu 12,707,600 kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari;

(vi) imeendelea na maandalizi ya utoaji Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu ambapo miswada 261 (Riwaya 53, Ushairi 85, Hadithi za Watoto 74, Tamthiliya 49) imepokelewa na inachambuliwa;

(vii) imeendelea na utoaji wa huduma za maktaba ambapo imewezesha kuwahudumia watumiaji 159,256 wakiwemo watumiaji wenye mahitaji maalumu, na kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii. Aidha, imeendelea na ujenzi wa Maktaba ya Mkoa wa Mwanza, na ukarabati wa Maktaba ya Mkoa wa Mara na Mtwara;

(viii) imeendelea kutoa huduma za maktaba kwa njia ya kidijitali na kuendelea kushiriki katika maonyesho ya kitaifa. Aidha, imeandaa toleo la tatu la Jarida la Bodi ya Huduma ya Maktaba Tanzania ili kuongeza uelewa kuhusu huduma na majukumu ya maktaba;

(ix) imefanya ufuatiliaji katika vyuo vya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi 18 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 9. Ufuatiliaji huo ulibaini uwepo wa mahitaji ya vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwemo vifaa vya kufundishia na kujifunzia, miundombinu isiyokidhi mahitaji, uelewa mdogo wa walimu na watumishi mwega kuhusu elimu jumuishi; na

(x) imewezesha ununuzi na ugawaji wa vifaa kwa ajili ya walimu na wakufunzi wenye mahitaji maalum kwa mchanganuo ufuatao; *Laptop* Zenye Program ya NVDA 286*, Laptops* 402, *Braille Note Touch Plus* 19, *Voice Recorder* 377, *Tablets (for sign language*) 196, *Everest D Braille Embosser* 5, *Sound amplifiers* 6, *Visual advanced assessment tool kit* 4, *Advanced hearing assessment kit* 4, *DUXBURY TRANSLATORSOFTWARE* 5, Perkins Brailler 130, *Braille Paper* 3,000, *Universal braille kit* 91, *Embosser Braille paper* 2,291, *Hearing Aids* 121, *CRUTCHES* 11, *Sun screen special lotion for person with albinism* 3,556, *Sun hats with UV Protection* 86, *Automated Wheel Chair* 2, *Wheelchair* 3, na *White Cane (Foldable*) 7.

Serikali imeendelea kufanya upimaji na tathmini ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi - PSLE, 2025 kwa watahiniwa **1,146,231** (wasichana ni 626,147 na wavulana ni 520,084) sawa na asilimia 97.77 ya watahiniwa **1,172,324** waliosajiliwa (wasichana 637,162 na wavulana 535,162) ambapo watahiniwa **937,581** (wasichana 508,477 na wavulana 429,104) walifaulu mtihani huo;

(ii) imeendesha upimaji wa Kidato cha 2 - FTNA kwa wanafunzi **819,023** (wasichana ni 461,322 na wavulana ni 357,701) sawa na asilimia 91.12 ya watahiniwa **898,835** waliosajiliwa (Wasichana 497,959 na Wavulana 400,876);

(iii) imeendesha upimaji wa kitaifa wa Darasa la IV – SFNA ,2025 kwa wanafunzi **1,490,384** (wasichana ni 780,591 na Wavulana ni 709,793) sawa na asilimia 94.10 ya wanafunzi 1,583,821 waliosajiliwa (wasichana 818,730 na wavulana 765,091);

(iv) imeendesha mtihani wa Kidato cha Nne - CSEE, 2025 kwa watahiniwa **570,079** (wasichana 303,959 na wavulana 266,120) waliosajiliwa; na

(v) imekamilisha usajili wa watahiniwa **126,479** kwa ajili ya mtihani wa kidato cha 6 ACSEE, 2026 ambapo Wasichana 62,409 na Wavulana 64,070 na Kwa watahiniwa **14,138** wa mtihani wa Ualimu ambapo Wasichana ni 9,122 na Wavulana ni 5,016 kwa mwaka 2026.

Serikali imeendelea kuboresha programu huria na masafa kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha vipindi vya ana kwa ana na programu huria na masafa kwa jumla ya wanafunzi 4,128 kama ifuatavyo; Astashahada 13, Astashahada Ufundi 1,310, Stashada 2,047, Stashahada ya Juu 408 na Shahada 350;

(ii) imeendelea kuboresha utoaji wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala na fursa za programu za elimu ya kisomo (kusoma na kuandika) kwa kutoa huduma za elimu kwa vijana na watu wazima waliokosa elimu kwa njia ya mfumo rasmi katika mikoa yote Tanzania Bara ambapo hatua ya I na II ya mitihani ya majaribio ilifanyika kwa wanafunzi 1,231;

(iii) imewezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,528 wanaosoma kwa njia ya ana kwa ana na huria na masafa. Kati ya hao, wanafunzi 125 ni wa ana kwa ana na 1,403 ni wa masafa;

(iv) imeratibu usimamizi wa mitihani ya wanafunzi 3,056 wanaosoma kwa njia huria na masafa, kati ya hao wanafunzi 1,224 wa Astashahada, 811 wa Stashahada na 1,021 wa Shahada. Aidha, wanafunzi 3,141 sawa na asilimia 72 walifanya mitihani ya majaribio ya muhula wa kwanza kati ya wanafunzi 4,337 waliosajiliwa. Vilevile, imesimamia mitihani kwa wanafunzi 892 wakiwemo wanafunzi 103 wa Astashahada, wanafunzi 569 wa Stashahada na wanafunzi 220 wa Shahada waliojiandikisha kupitia programu za ana kwa ana;

(v) imewajengea uwezo walimu na watendaji (viongozi) wa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Shule – IPOSA wa namna ya kupata wanufaika wa mradi, kufundisha, kuanzisha na kuendeleza vituo vya IPOSA katika wilaya za Kasulu, Kakonko na Sumbawanga;

(vi) imeendelea na ukamilishaji ujenzi wa vituo 3 vya mfano vya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Shule – IPOSA katika Mkoa wa Manyara, Tanga na Shinyanga ambavyo ujenzi wake uko katika hatua za ukamilishaji;

(vii) imekamilisha ujenzi wa madarasa, vyumba vya watoto na vyoo na inaendelea na ujenzi wa majengo ya utawala unatarajiwa katika Mkoa wa Simiyu, Singida, Njombe na Geita; na

(viii) imekamilisha ukarabati wa hosteli katika kampasi ya Morogoro na imeanza ujenzi wa hosteli katika Mkoa wa Katavi, Mara na Mbeya. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli katika Mkoa wa Iringa.

### 3.4. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu

Serikali imeendelea kuimarisha fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu na stashahada kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi **102,800** wa mwaka wa kwanza ambapo shahada ya kwanza **93,708,** Shahada za juu **309** na diploma **8,783** Aidha, imetoa mikopo kwa wanafunzi **173,232** wanaoendelea na masomo ambapo shahada ya kwanza **167,362**, Shahada za juu **49** na diploma **5,821;**

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza **934** na wanaoendelea **844** kupitia **SAMIA *Scholarship*;**

(iii) imeendelea kutoa ufadhili wa masomo ya shahada ya umahiri kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo bora duniani katika eneo la sayansi ya nyuklia. Lengo likiwa ni kuongeza watalaamu katika eneo hilo nchini kupitia **SAMIA *Scholarship Extended*;**

(iv) imeanzisha ufadhili wa **SAMIA *Extended DS/AI+*** katika ngazi ya Shahada ya Kwanza ambapo wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu wa kidato cha sita katika fani za sayansi (PCM, PGM na PMC) wamechaguliwa kusoma fani za Sayansi Data, Akili Unde na Sayansi Shirikishi. Aidha, wanufaika wa ufadhili huu wamemaliza kambi ya maarifa kwa miezi 10 katika taasisi ya NM-AIST kwa ajili ya kupewa usaidizi wa kitaalamu kupitia matayarisho ambapo wanafunzi 16 wataondoka mapema mwezi Februari, 2026 kuanza masomo katika Chuo Kikuu cha Johannesburg nchini Afrika Kusini na wanafunzi wengine wameshafanya matayarisho muhimu ya kuwawezesha kujiunga na vyuo vikuu bora nje ya nchi.

(v) imeanzisha ufadhili wa masomo wa Samia (Samia Scholarship Extended) katika ngazi ya Shahada ya Uzamili kwenye masomo ya Data Science, Artificial Intelligence, Cybersecurity, Machine Learning na kozi nyingine za TEHAMA. Ufadhili huu utatolewa katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) Arusha au Kampasi ya Zanzibar ya India Institute of Technology (IIT), Madras;

(vi) imekusanya jumla ya Shilingi **114,970,726,780.25** kutokana na mikopo iliyoiva sawa na asilimia **54.7** ya lengo la kukusanya **Shilingi Bilioni 210,273,850,000**. Aidha, mbinu mbalimbali za kimkakati kama vile kampeni za uhamasishaji, ubainishaji na utozaji bili kwa walengwa zinatumika; na

(vii) imetoa Mafunzo ya Vitendo vya Uwandani kwa wanafunzi wa mwaka 2006 katika klasta ya tatu wakiwemo wanafunzi wa Uhandisi kutoka Shule ya Uhandisi na Teknolojia, Wanafunzi wa cheti cha Uongozaji Watalii na Uwindaji (CTGHO), wanafunzi kutoka Chuo cha Misitu, Wanyamapori na Utalii. Mafunzo hayo yalianza tarehe 28 Julai, 2025 hadi tarehe 19 Septemba, 2025 kupitia Chuo kikuu cha Sokoine.

Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za elimu ya Juu na Taasisi za Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu ambapo hatua iliyofikiwa ya ujenzi ni kama ifuatavyo: kampasi ya Chuo Kikuu Ardhi - Sengerema asilimia 26; kampasi ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia - Tabora asilimia 59; kampasi ya Chuo Kikuu Dodoma - Njombe asilimia 37; kampasi ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili - Kigoma asilimia 33; kampasi ya Mzumbe - Tanga asilimia 65; kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Lindi asilimia 60; Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Mjini Magharibi ujenzi umekamilika; kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Kagera asilimia 77; kampasi ya Chuo cha Kikuu cha Ushirika Moshi - Shinyanga asilimia 98; kampasi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - Rukwa ujenzi umekamilika; kampasi ya Chuo cha Uhasibu Arusha - Ruvuma asilimia 22; kampasi ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha - Mwanza asilimia 65; kampasi ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha - Simiyu asilimia 63; kampasi ya Chuo cha Uhasibu - Singida asilimia 31; kampasi ya Chuo cha Uhasibu - Mwanza asilimia 57; na kampasi ya Chuo cha Kilimo cha Sokoine - Katavi asilimia 61;

(ii) imeendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 48. Aidha, imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa kila bweni. Ujenzi wa bweni A umefikia asilimia 89 na bweni B asilimia 25. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa majengo manne (Jengo la Sayansi, Midia anuai na Elimu ya Mahitaji Maalum, Hosteli za wanafunzi wenye mahitaji maalumu na maabara ya fizikia) ambapo ujenzi wa jengo la hosteli na maabara ya fizikia umefikia asilimia 80 na ujenzi wa jengo la sayansi na midia anuai na elimu ya mahitaji maalum umefikia asilimia 80 katika Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(iii) imeendelea na ujenzi wa majengo manne (4) ambayo ni: jengo la maabara ya matumizi anuwai (Multipurpose Laboratory) ambapo ujenzi umefikia asilimia 94; jengo la studio asilimia 95; jengo la karakana asilimia 92; na jengo la madarasa asilimia 91 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 6,135 na watumishi 73 kwa wakati mmoja. Aidha, imekamilisha ukarabati wa miundombinu ya TEHAMA, na inaendelea na ukarabati wa madarasa 76 na mabweni matatu (3) ya wanafunzi katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu Ardhi;

(iv) imeendelea na kazi ya uunganishaji wa miundombinu ya maji katika mabweni ya ndaki ya elimu pamoja na kuweka miundombinu ya maji katika mabweni matatu yaliyopo ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu angavu katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(v) imeendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala lenye uwezo wa kuchukua watu 1,800 kwa wakati mmoja. Aidha, imeendelea na ujenzi wa jengo la taaluma Tegeta ambapo ujenzi upo katika hatua ya msingi. Vilevile, imeendelea na ukarabati wa hosteli kampasi kuu katika Chuo Kikuu Mzumbe;

(vi) imeendelea na ujenzi wa majengo matatu (3) katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ambapo ujenzi wa jengo la TEHAMA umefikia asilimia 88.5, jengo la hostel asilimia 81 na jengo la taaluma asilimia 74.2. Aidha, imenunua vifaa mbalimbali vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na imeendelea

na ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 67;

(vii) imeendelea na ukarabati wa jengo la utawala *wing* A na B ambapo ukarabati umefikia asilimia 85 katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Aidha, imeendelea na ujenzi wa ofisi ya taaluma katika kituo cha uratibu Pemba ambapo ujenzi umefikia asilimia 45;

(viii) imeendelea kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza wa Hosteli yenye ghorofa nne (4) katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- NM-AIST lenye *wings* tano (5) ambapo ujenzi umefikia asilimia 80;

(ix) imekarabati hosteli tano (5) za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya- MUST;

(x) imekamilisha upanuzi wa Hosteli ya Dkt. J.P.J. Magufuli (Blocks A na E) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, inaendelea na ufungaji wa vitanda 200 kati 288 vinavyohitajika;

(xi) imeendelea na ujenzi wa jengo la usalama katika Kampasi ya Solomon Mahlangu kwa ajili ya kuboresha huduma mbalimbali za usalama chuoni ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Aidha, imeendelea na ukarabati wa miundombinu katika Bweni Na. 1 na 7 katika kampasi ya Edward Moringe na bweni "Unit 2" katika kampasi ya Solomon Mahlangu na nyumba tano za watumishi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; na

(xii) imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu - HESLB Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 76.39.

Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na uthibiti wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kutekeeza yafuatayo:

(i) imeratibu maombi ya wanafunzi 170,916 walioomba kujiunga na Elimu ya Juu kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika vyuo vya elimu ya juu nchini kwa mwaka wa masomo 2025/26. Kati ya maombi hayo, jumla ya waombaji 159,010 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini;

(ii) imetathmini Tuzo 1,636 za waombaji waliosoma vyuo vikuu vya nje ya nchi, Kati ya hizo, tuzo 1,240 zilikidhi vigezo na kutambuliwa kama ifuatavyo: post Certificate (1), Cheti (6), Stashahada (63), Shahada (681), Postgraduate certificate (14), Shahada ya Uzamili (394) na Shahada ya Uzamivu (81);

(iii) imeratibu maombi ya wanafunzi 1,313 walioomba udahili katika Vyuo Vikuu vya nje ya nchi na kuwapatia hati ya kutokuwa na pingamizi (No Objection Certificate) wanafunzi 1,246 kama ifuatavyo: Cheti (1), Diploma (124), Shahada (1,006), Shahada ya Uzamili (100), na Shahada ya Uzamivu (15);

(iv) imefanya tathmini ya programu 461 kati ya hizo, programu 233 zilipatiwa ithibati kama ifuatavyo: Astashahada (7), Shahada (193), Shahada ya Uzamili (23), na Shahada ya Uzamivu (10);

(v) imefanya tathmini ya maombi ya wakala nne (4) wanaohusika kupeleka wanafunzi vyuo vya nje ya nchi, kwa lengo la kufanya kaguzi, kuzisajili au kuhuisha usajili. Taasisi hizo ni: Tolu Study Abroad, QETC Education and Training Consultancy Limited, Goexpro World Travel, na ROZAC Company Limited.

(vi) imeandaa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za watanzania wanaoenda kusoma vyuo vya nje ya nchi kupitia Wakala waliosajiliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); na

(vii) imekamilisha Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu wa Mwaka 2025/26- 2029/30. Lengo ni kuimarisha mifumo na miundombinu itakayowezesha ufikiaji wa usawa wa kijinsia na Elimu Jumuishi katika Taasisi za Elimu ya Juu.

Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano baina ya vyuo vyetu vikuu vya ndani na vyuo vikuu vya nje kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imepokea jumla ya vijana wa mafunzo kwa vitendo 19 na wakufunzi 5 kutoka nchi mbalimbali zikiwemo India, Palestina, Yemen, Tunisia, Ujerumani, Austria, Jamhuri ya Czech, Uhispania, Uswisi na Iran. Wanafunzi hao walipata

mafunzo katika taasisi mbalimbali zikiwemo MUHAS, MUST, NECTA na OUT. Lengo la programu ni kuwawezesha kupata uzoefu wa kimataifa kwa vitendo katika fani za afya na sayansi shirikishi, sayansi ya viumbe, sayansi ya tiba, sayansi ya kompyuta na maeneo mengine yanayohusiana. Pia, programu ililenga kuboresha ujuzi wao katika kuwahudumia makundi maalum katika sekta ya elimu kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; na

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 187 kutoka nchi mbalimbali kama ifuatavyo: Urusi (90), China (49), Hungaria (21), Jumuiya ya Madola (11), Algeria (8), Morocco (4) na Mauritius (4). Aidha, imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Serikali imeendelea kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi waliopo katika Vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha mafunzo ya watumishi 114 (mafunzo ya muda mrefu 33 na muda mfupi 81) katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(ii) imetoa ufadhili wa masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 37 (Shahada ya kwanza 2, Umahiri 18 na Uzamivu 17) kupitia Chuo Kikuu Mzumbe;

(iii) imetoa mafunzo kwa wanataaluma 75 kuhusu namna ya kutumia teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi kuhusu kuboresha utoaji wa masomo-mtandao kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam- DUCE;

(iv) imewezesha wafanyakazi 131 kuendeleza masomo ya muda mrefu: 49 katika ngazi ya uzamili, 79 wa uzamivu, na 3 wa shahada ya kwanza. Kati yao, 104 ni wa kada ya kitaaluma na 27 wa utawala katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;

(v) imewezesha mafunzo kwa watumishi 98 (muda mfupi 85 na muda mfupi 13) kati yao wanataaluma 70 na watumishi waendeshaji 15 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi – MoCU;

(vi) imeendelea kutoa ufadhili kwa watumishi 41 katika kozi za muda mrefu na muda mfupi 210 katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;

(vii) imeendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 11 wakiwemo wanataluma 4 (wanaume 2 na wanawake 2) na wasio wanataaluma 7 (wanaume 2 na wanawake 5) katika Chuo Kikuu Ardhi; na

(viii) imeendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 81 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo jumla ya wafanyakazi 43 ni shahada za uzamili, 37 ni shahada za uzamivu moja (1) ni shahada ya awali; na

(ix) imetoa mafunzo ya mda mfupi kwa wafanyakazi 285 wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (wanaume 152 na wanawake 133). Aidha, wafanyakazi 20 (wanaume 10 na wanawake 10) wamepewa ufadhili wa masomo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili.

Serikali imeendelea kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Taasisi za Elimu ya juu kwa kuziwezesha upatikanaji wa vifaa kama ifuatavyo:

(i) imewezesha ununuzi wa samani kwa ajili ya madarasa na ofisi katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia Mwalimu Nyerere -MNUAT; na

(ii) imesajili hifadhidata mbili za rasilimali za Maktaba ambazo ni *EBSCOhost* na *Emerald Insight* ili kuboresha upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia kwa njia ya kielektroniki kwa wanafunzi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### 3.5. Kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

Serikali, imeendelea kufanya tafiti mbalimbali za elimu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 kama ifuatavyo:

(i) imefanya utafiti kuhusu tatizo la mdondoko wa wanafunzi katika Shule za Msingi na Sekondari Nchini (Understanding the Problem of School Dropouts in Tanzania's Primary and Secondary Schools - 2025). Aidha, utafiti husika umechambua kwa kina sababu za wanafunzi kuacha masomo na kutoa mapendekezo yatakayoisaidia Wizara na wadau wa elimu kuweka mikakati na afua za kudhibiti tatizo la mdondoko wa wanafunzi shuleni;

(ii) imefanya Tathmini ya Matokeo ya Utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Kuwarejesha Shuleni Wanafunzi waliokatisha Masomo yao kwa Sababu Mbalimbali (Impact Assessment of School Re-Entry Policies in Mainland Tanzania - 2025). Aidha, tathmini husika imesaidia Wizara kubaini sababu zilizoleta mafanikio katika utekelezaji wa sera na miongozo husika na changamoto zinazoweza kukwamisha utekelezaji wake;

(iii) imefanya utafiti kuhusu Mnyororo wa Ugawaji wa Vitabu vya Kiada Nchini (Tanzania Textbook Supply Chain – Practices, Experiences and Opportunities) uliolenga kufanya tathmini ya kina kuhusu utaratibu wa kubainisha mahitaji, kununua, kusambaza, matumizi na ufuatiliaji wa vitabu vinavyotolewa na Serikali. Aidha, utafiti husika umesaidia Wizara na Wadau wa Elimu kubaini changamoto zilizopo pamoja na mikakati inayoweza kuboresha ufanisi katika upatikanaji na matumizi bora ya vitabu vya kiada katika sekta ya elimu;

(iv) imefanya tafiti kuhusu kuongeza ufanisi katika uongozi na usimamizi wa shule kwa walimu wakuu wa sekondari na kutambua mahitaji yao kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - ADEM;

(v) imeratibu miradi ya tafiti 163 kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH katika maeneo ya kilimo, afya, maji, nishati, uchumi wa bluu,

mabadiliko ya tabia nchi, elimu, viwanda na teknolojia mpya ili kutatua changamoto zinazokabili sekta; na

(vi) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti 312 kupitia Taasisi za Elimu ya juu na vyuo vya Elimu ya ufundi katika maeneo ya ardhi, ujenzi, maji, tabianchi, mazingira, kilimo, afya, elimu, viwanda, sayansi ya jamii, teknolojia, biashara, ushirika na uwekezaji. Aidha, imeendelea na kazi za utafiti kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Sayansi za Kilimo cha Japan (JIRCAS) kuhusu maendeleo ya teknolojia ya kuwezesha ufanisi wa matumizi ya maji ya mvua na umwagiliaji rahisi kupitia Chuo cha Ufundi Arusha.

Serikali imeendelea kuimarisha maendeleo na mchango wa utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa yafuatayo:

(i) imeratibu ukamilishaji wa tathmini ya Muundo, Majukumu na Utendaji wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Comprehensive Review of Forms, Functions and Performance of COSTECH);

(ii) imeratibu uanzishaji wa Madawati ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) katika Halmashauri 13 na matarajio ni kuwa hadi ifikapo Juni 2026 madawati hayo yatakuwa yameshaanzishwa katika jumla ya Halmashauri 72 nchini;

(iii) imeanza utekelezaji wa Mfuko wa "Samia Commercialization Fund" kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), unaolenga kutoa mikopo nafuu kwa wabunifu ili kuwezesha ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia zao. Katika awamu ya kwanza, jumla ya wabunifu saba (7) wamenufaika na Mfuko huu. Miongoni mwa bunifu zilizosaidiwa ni pamoja na uchakataji na usambazaji wa asali bora kwa masoko ya nje, uchakataji na usambazaji wa mafuta ya mawese kwa masoko ya nje, pamoja na mfumo wa kudhibiti foleni katika hospitali;

(iv) imesimamia miradi 93 ya ubunifu ikijumuisha miradi 19 ya washindi wa MAKISATU na 60 ya utafiti ambayo imelenga kutoa ufumbuzi wa changamoto zinazokabili sekta mbalimbali muhimu ikiwemo kilimo, usalama wa chakula, maji, afya, uchumi wa buluu, mabadiliko ya tabianchi, teknolojia mpya, elimu ya hisabati, ujenzi, usafirishaji, nishati, usalama, uzalishaji na sekta za viwanda;

(v) imeendeleza bunifu saba (7) kupitia Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya -MUST ambazo zilionyeshwa katika maonesho mbalimbali, bunifu hizo ni; Multitenant Electric Meter, Hydrogen Fuel Electrolyser, Blind Stick, Electronically Controlled Incubator, Solar-Powered Grass Cutter, Pedal Washer Machine, and Aquaponic Fertilizer Production System. Ubunifu huu unatarajiwa kuwasilishwa kwa ajili ya ushirikiano na viwanda mbalimbali, kwa lengo la kuendeleza utafiti na kuufanya ubunifu kuwa bidhaa ya kibiashara. Ubunifu huu unalenga kuboresha maisha ya kila siku kwa kushughulikia changamoto muhimu katika maeneo ya usimamizi wa nishati, uzalishaji wa mafuta safi, teknolojia saidizi, kilimo bora na mashine endelevu;

(vi) imeratibu uzinduzi na utekelezaji wa Mpango wa Stipendi ya SAMIA *Scholarship Extended* (SSE DS/AI+) katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - NM-AIST. Wanafunzi 50 bora wa kidato cha sita waliandikishwa kwenye bootcamp, na Mwongozo wa Uendeshaji wa Programu ulisasishwa. COSTECH pia ilishirikiana na wadau wa maendeleo na vyuo vikuu kama Queen’s University Belfast na IIT Madras kwa fursa za masomo ya kimataifa;

(vii) imeandaa rasimu ya kiunzi cha Kitaifa cha maandalizi ya Vyuo 12 vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) kuwa vituo vya teknolojia vya kimkoa/kikanda;

(viii) imetoa mafunzo kuhusu Moduli za Uandaaji wa Maudhui ya Kidijitali kwa wahadhiri 126 kwa lengo la kuwawezesha kutumia kwa ufanisi majukwaa 40 ya kidijitali kwa ajili ya ushirikishaji wa wanafunzi na ufundishaji kwa kutumia zana kama Google Meet, Zoom, Google Classroom, pamoja na majukwaa mengine ya ufundishaji na ujifunzaji mtandaoni. Aidha, Programu ya Mafunzo ya Ufundishaji Jumuishi wa Ubunifu (Innovative Blended Pedagogy) iliendeshwa kwa wafanyakazi wa Ndaki ya MRCC ikiwa na jumla ya washiriki 22 ikilenga kuunganisha mikakati bunifu ya ufundishaji inayochanganya mbinu za kawaida na za kidijitali;

(ix) imeanzisha Multimedia Studio ili kusaidia na kuimarisha utekelezaji wa mafunzo ya kielektroniki katika Ufundishaji na ujifunzaji, pia imeanzisha

mpango wa Kufundisha na Kujifunzia Dijitali (DTLU) ambao umeidhinishwa wakati wa mkutano wa COPD;

(x) imekamilisha na kuidhinisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuhamasisha mchango wa Diaspora katika shughuli za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) (National Strategy for Promoting Diaspora Engagement in Education and STI);

(xi) imebiasharisha bunifu tano (5) ikiwemo mashine ya kusafishia mafuta, mashine ya kukaanga nafaka mbalimbali, taa za urembo, mashine ya kuchakata chakula cha wanyama pamoja na jiko la kutumia nishati safi kupitia VETA;

(xii) imewasilisha hati miliki saba (7) za bunifu BRELLA, ambapo hatimiliki mbili (2) zimeshatangazwa na tano (5) zinaendelea kufanyiwa kazi. Hatimiliki hizo zinatarajiwa kuendelezwa na kugeuzwa kuwa kampuni changa (startups) na kupitia mchakato wa uhaulishaji teknolojia. Bunifu hizo ni pamoja na: Mfumo wa kiteknolojia wa kufuatilia ubora wa hewa katika mkoa wa Dar es Salaam;Filamu ya kibayolojia kwa ajili ya fungashia bidhaa, inayotengenezwa kwa kutumia mwani aina ya *Ulva lactuca;* Mfumo mahiri wa kifaa cha mkononi kwa ajili ya huduma za LUKU; Programu ya Sitiolojia ya Macho inayotumia Akili Mnemba (AI) kubaini tatizo la Diabetic Retinopathy;Mfumo wa GEOAMIS kwa uchakataji wa data na utabiri wa mafuriko; Roboti ya Akili Mnemba (AI) Rafiki kwa ajili ya elimu na huduma shirikishi kwa wazee; na Kifaa cha mkononi cha kufuatilia na kutabiri ukame;

(xiii) imekamilisha na kuwasilisha mapendekezo ya kuanzishwa kwa Jukwaa la Kitaifa la Uratibu wa Masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Nchini (Tanzania National Science, Technology and Innovation Platform-TANZSTIP) katika kikao cha Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu (Inter-Ministerial Technical Committee- IMTC); na

(xiv) imeshiriki Wiki ya 11 ya Uhandisi Afrika ya UNESCO pamoja na Mkutano wa 9 wa Uhandisi Afrika (AEC) uliofanyika Kampala-Uganda, ukiwa na kaulimbiu "Kutekeleza mageuzi ya kijamii na kiuchumi Afrika kupitia ubunifu na teknolojia ya Uhandisi.

Serikali imeendelea kutoa machapisho na huduma ya ushauri kwa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa wahariri wa majarida 197, wakaguzi, na watafiti kuhusu mbinu bora za uchapishaji wa kisayansi. Tukio ambalo liliendeleza Mswada wa Mwongozo wa Kitaifa wa Kutambua na Kukuza Maendeleo ya Majarida ya Kisayansi na kuimarisha ushirikiano na mashirika ya kimataifa ya kuorodhesha majarida;
(ii) imetoa jumla ya machapisho 629 ya kitaaluma katika majarida ya kitaifa na kimataifa kupitia Taasisi za Elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi ili kuongeza maarifa katika jamii kuhusu namna ya kutatua changamoto mbalimbali; na
(iii) imeendelea kutoa huduma ya ushauri 114 katika maeneo yafuatayo; ugani, vyama vya ushirika, matumizi ya udongo, mawe na nyenzo zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali, pamoja na kupima ubora wa maji na pia ikihusisha Usanifu na Usimamizi wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati michoro ya usanifu, maandalizi ya makadirio ya gharama za ujenzi.

Serikali imeendelea kudhibiti na kukuza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(iv) imepima jumla ya sampuli 31,739 kati ya sampuli 25,000 za vyakula na vifaa vya mlolongo wa chakula zilizolengwa ikiwa ni sawa na asilimia 126.9 ya lengo ili kubaini uwepo wa uchafuzi wa mionzi. Kati ya sampuli hizo, sampuli 7,763 zilihusu bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, sampuli 20,951 zilihusu bidhaa za kusafirisha nje, na sampuli 3,025 zilihusu mbolea, tumbaku na wasambazaji wa vifaa vya mlolongo wa chakula;
(v) imefanya upimaji wa uthibitisho wa vifaa 40 vilivyotoka Tume ya Nguvu ya Atomu 22, Chrysos Corporation 8, PCS Energy Company 2, MSA Laboratories 2, Tanzania Steel Pipe 1, Bugando Medical Centre 1, Nuctech Company Limited 1, Bulyanhulu Medical Centre 1, GO Shuqing 1 na Bottles Company Limited 1;
(vi) imepima wafanyakazi 1,358 wanaofanya kazi katika mazingira yenye mionzi kutoka katika vituo 226 ikilinganishwa na lengo la kupima wafanyakazi 1,050

katika kipindi cha kuanzia Julai na Desemba 2025. Aidha, wafanyakazi wote waliofuatiliwa walipokea dozi za mionzi kati ya milisiveti 0.1 hadi 3.0 (mSv), ambazo zipo ndani ya kikomo cha kisheria kinachokubalika cha milisiveti 5 kwa kipindi cha miezi sita;

(vii) imepima jumla ya sampuli 244 za mazingira kwa ajili ya kubaini kiwango cha mionzi kwa kutumia vitambua mionzi .Sampuli hizo zilitolewa na wanafunzi wa vyuo vikuu, makampuni binafsi na watafiti wa kisayansi. Hii ni sawa na utekelezaji wa asilimia 61 ikilinganishwa na lengo la kuchambua sampuli 400 za mazingira lililopangwa kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025;

